**JEDWALI LA MAREKEBISHO LITAKALOWASILISHWA NA MH. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA, WAZIRI MKUU WAKATI WA KUSOMA KWA MARA YA PILI MUSWADA WA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAAFA WA MWAKA 2022**

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 99 (10))*

Muswada unaoitwa "Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022" unarekebishwa kama ifuatavyo:

**A:** Katika Ibara ya 2 kwa kufuta tafsiri ya msamiati "usimamizi wa maafa" na badala yake kuweka tafsiri ifuatayo:

"usimamizi wa maafa" inajumuisha hatua zinazochukuliwa kuzuia na kupunguza madhara ya majanga, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali endapo maafa yanatokea kwa kuzingatia sera, sheria na miongozo;";

**B:** Katika Ibara ya 6-

(a) katika ibara ndogo ya (1) (a), kwa kuongeza maneno "au kuamuru watu kubaki katika maeneo salama" baada ya neno 'hatarishi';

(b) katika ibara ndogo ya (1) (c), kwa kufuta maneno "mtu yeyote, idara au taasisi" na badala yake kuweka maneno "taasisi za umma"; na

(c) katika ibara ndogo ya (2), kwa kufuta neno "utekekezwaji" na badala yake kuweka neno "utekelezaji".

**C:** Katika Ibara ya 7(2) kwa kufuta aya ya (g) hadi (u) na badala yake kuweka aya zifuatazo:

"(g) Waziri mwenye dhamana ya afya;

(h) Waziri mwenye dhamana ya kilimo na usalama wa chakula;

(i) Waziri mwenye dhamana ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari;

(j) Waziri mwenye dhamana ya ujenzi na usafirishaji;

(k) Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya jamii;

(l) Waziri mwenye dhamana ya tawala za mikoa na serikali za mitaa; na

(m) Waziri mwenye dhamana na maji.";

**D:** Katika Ibara ya 9(2) kwa kufuta aya ya (f) hadi (w) na badala yake kuweka aya zifuatazo:

"(f) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana afya;

(g) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari;

(h) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi;

(i) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya kilimo na usalama wa chakula;

(j) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya maji;

(k) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya mambo ya ndani ya nchi;

(l) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya ujenzi na usafirishaji;

(m) Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania;

(n) Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; na



OFFICE OF THE CLERK OF THE NATIONAL ASSEMBLY
RECEIVED
13 SEP 2022
P. O. Box 941
DODOMA

(p) Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania.";

**E:** Katika Ibara ya 15-

(a) katika ibara ndogo ya (2) kwa kufuta aya ya (e) hadi (q) na badala yake kuweka aya zifuatazo:

"(e) Afisa Operesheni Mkoa wa Jeshi la Polisi Tanzania;

(f) Afisa Operesheni Mkoa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(g) Mshauri wa Mgambo Mkoa;

(h) Mkuu wa taasisi inayohusika na barabara za vijijini na mijini katika ngazi ya Mkoa;

(i) Mkuu wa taasisi inayohusika na barabara kuu na za mikoa katika Mkoa;

(j) Mkuu wa taasisi inayohusika na huduma za maji na usafi wa mazingira katika Mkoa;

(k) Mkuu wa taasisi inayohusika na usanifu na ubora wa majengo katika Mkoa; na

(l) Mratibu wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania katika Mkoa.";

(b) kwa kuongeza baada ya ibara ndogo ya (2) kama ifuatavyo-

"(3) Katibu Tawala Msaidizi anayehusika na uratibu na mipango atakuwa Katibu wa Kamati.";

(c) kuifanya ibara ndogo ya (3) kuwa ya (4);

**F:** Katika Ibara ya 19 (2) kwa kufuta aya ya (c) hadi (o) na badala yake kuweka aya zifuatazo:

"(c) Afisa Operesheni Wilaya wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(d) Mkuu wa Upelelezi Wilaya wa Jeshi la Polisi Tanzania;

(e) Mkuu wa taasisi inayohusika na barabara za mijini na vijijini katika Wilaya;

(e) Mkuu wa taasisi inayohusika na huduma za maji na usafi wa mazingira katika Wilaya;

(g) Mratibu wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania katika Wilaya; na

(h) Kamishna wa Skauti Wilaya.";

**G:** Katika Ibara ya 21-

(a) katika aya ya (b) kwa kuongeza maneno "au kuamuru watu kubaki katika maeneo salama" baada ya neno "Wilaya"; na

(b) katika aya ya (c) kwa kuongeza maneno "rasilimali za umma kama vile" baada ya neno "kutumia";

**H:** Katika Ibara ya 24 (1) kwa kufuta maneno "Baraza la Kijiji lililoundwa chini ya Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) litakuwa" yaliyopo mwanzoni mwa ibara hiyo na badala yake kuweka maneno "Halmashauri ya Kijiji iliyoundea chini ya sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (mamlaka za Wilaya) itakuwa";

**I:** Katika Ibara ya 29 kwa kufuta maelezo ya pembeni na badala yake kuweka maneno "Taratibu za uendeshaji wa Kamati";

**J:** Katika Ibara ya 32(1) kwa kufuta neno "kupitia" lililopo kati ya maneno "tangazo" na

"Gazeti" na badala yake kuweka neno "katika";

**K:** Katika Ibara ya 36 (1) kwa kufuta maneno "milioni moja au kifungo kisichozidi mwaka mmoja" na badala yake kuweka maneno "laki tatu na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi mwaka mmoja.";

**L:** Kwa kuongeza Ibara mpya ya 38 kama ifuatavyo:

"Adhabu ya jumla

**38.** Mtu yeyote anayekiuka masharti yoyote ya Sheria hii, na iwapo hakuna adhabu mahsusi iliyotamkwa, atakuwa anatenda kosa, na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tatu na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua mwezi mmoja na kisichozidi mwaka mmoja au vyote."; na

**M:** Kwa kubadili mpangilio wa Ibara za 38 hadi 40 na kuwa Ibara za 39 hadi 41 mtawalia.

Dodoma,
.........................., 2022

**KMM**
*WM*